THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KCPE 2001

# KISWAHILI

## SEHEMU YA PILI: INSHA

**Muda: Dakika 40**

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu andika Namba Yako kamili ya mtihani, Jina lako na Jina la Shule yako.

Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Insha**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu juu ya kichwa kifuatacho:

Umeshinda shilingi milioni moja katika mchezo wa bahati nasibu. Eleza utakavyozitumia pesa hizo.

# KISWAHILI

## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Maswali 1 mpaka 15.**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Yamkini baadhi ya wanafunzi hawapendi michezo, ni muhimu kukumbuka kuwa michezo __1__ manufaa mengi sana kwao. __2__ kusema kweli michezo __3__ watoto __4__ nzuri ya kujifunza mambo mengi. Pili, michezo husaidia viungo vyote mwilini kuwa imara na __5__ afya. Pia akili hufanya kazi __6__ zaidi baada ya kupumzika wakati wa michezo. Isitoshe, michezo huwawezesha wanafunzi kujuana, kupendana, kusaidiana na __7__. Moyo huo wa udugu __8__ msingi wa taifa lenye umoja.

1. A. zina B. una C. yana D. ina
2. A. Ama B. Ati C. Bila D. Wala
3. A. huwapaza B. hupata C. huwapa D. huwapasha
4. A. ruhusa B. fursa C. nyakati D. radhi
5. A. vyenye B. zenye C. yenye D. wenye
6. A. jema B. vyema C. mwema D. wema
7. A. kushukiana B. hushukiwa C. hushikiana D. kushirikiana
8. A. ndio B. ndiyo C. ndiye D. ndiwe

Dhana ya uhifadhi wa mazingira sio __9__ kwetu sisi Waafrika hata kidogo. Tangu __10__ tulikuwa tukipanda na __11__ miti ya kila aina kwa matumizi tofauti kama vile dawa, kivuli, chakula na __12__. Shughuli hii ni __13__ __14__ wanadamu __15__ duniani.

9. A. geni B. ngeni C. mgeni D. ugeni
10. A. wakati B. mwakani C. jadi D. jana
11. A. kukuza B. kukua C. kukuzia D. kukuzwa
12. A. nyingi B. mengi C. mengineyo D. nyinginezo
13. A. bidii B. wajibu C. nia D. muhimu
14. A. zetu B. zenu C. lenu D. wetu

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.**

16. Aksami hii $^4/_5$ huitwa
    A. khumusi tano
    B. khumusi nne
    C. robo tano
    D. thuluthi nne.

17. Nilinyeshewa nikalowa maji
    A. chubwi
    B. Chakari
    C. Chepechepe
    D. Chururu

18. Kutokana na jina mlio tunapata kitenzi
    A. mlia
    B. mlizi
    C. kilio
    D. lia

19. Mablanketi ishirini pamoja huitwa _______ moja ya mablanketi.
    A. korija
    B. darzeni
    C. bunda
    D. jozi

20. Panga vifungu vifuatavyo ili vilete maana moja kamili
    (i) alipelekwa hospitali
    (ii) wala hatukufahamu
    (iii) aliugua nini
    (iv) hatukuelezwa kuwa
    A (ii) (iv) (i) (iii)
    B. (i) (iv) (iii) (ii)
    C. (iv) (i) (ii) (iii)
    D. (iii) (iv) (ii) (i)

21. Maana ya 'ungalifika ungaliniona' ni
    A. ulifi lakini hukuniona
    B. hukufika na hukuniona
    C. hukufika ila uliniona
    D. ulifika na uliniona.

22. Katika kamusi maneno hupangwa kulingana na abjadi yaani a, b, c, d, e na kuendelea. Ni orodha ipi ya maneno iliyopangwa vizuri?
    A. Kionjamchuzi, Kipaimara, Kipandikizo, Kipimajoto.
    B. Mamlaka, Mamia, Maliwazo, Mandhari.
    C. Somo, Sononeka, Shamrashamra, Staftahi.
    D. Urafiki, Uwaziri, Uvumbuzi, Uraia.

23. Chagua msemo wa taarifa ufaao wa sentensi 'Njoo haraka twende sokoni,' alimhimiza.
    A. Mama alimhimiza kuwa, 'njoo twende sokoni'
    B. Mama alimhimiza aje haraka twende sokoni.
    C. Mama alimhimiza 'twende sokoni haraka.'
    D. Mama alimhimiza amfuate haraka waende sokoni.

24. Ni kiunganishi kipi kilicho sahihi? Mwalimu alishindwa kulijibu hilo swali _______ mimi?
    A. bali
    B. wala
    C. sembuse
    D. licha.

25. Giza lilitoweka kukaanza kuwa _______ na kukapendeza.
    A. kweupe
    B. peupe
    C. weupe
    D. mweupe

26. Mtoto wa ndege anaitwa _______
    A. kifaranga
    B. kimatu
    C. kiweto
    D. kinda

27. Chagua sentensi iliyo sahihi kisarufi.
    A. Habari ambayo zilitufikia zilitushangaza.
    B. Habari ambazo zilitufikia zilitushangaza.
    C. Habari ambazo zilizotufikia zilitushangaza.
    D. Hahari ambao ilitufikia ilitushangaza.

28. Maana ya 'tuliimbiana' ni
    A. aliniimba nami nikamuimba
    B. aliimba nami nikaimba
    C. Aliniimbia nami nikamwimbia
    D. Aliwaimba nami nikawaimba.

29. Onyesha sentensi iliyo na ki ya masharti
    A. Nilikuwa nikienda sokoni alipowasili.
    B. Anatembea kivivu.
    C. Kile kitoto ni cha nani?
    D. Nikimwona nitamsalimu.

30. Chagua sentensi iliyopangwa vizuri zaidi.
    A. Wewe utakuja kwetu siku gani?
    B. Siku gani kwetu wewe utakuja?
    C. Kwetu siku gani utakuja wewe?
    D. Wewe kwetu siku gani utakuja?

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.**

Baada ya uhuru, Kenya ilihitaji kuikweza lugha moja ya kiasili kuwa lugha ya taifa. Wakenya hawakutaka kuitumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya taifa. Hii ilionekana kuwa lugha ya kikoloni na kigeni. Hali ya kuwepo lugha nyingi nchini ilitatiza uchaguzi wa lugha moja. Kila kabila lilitarajia lugha yake kuchaguliwa, jambo ambalo lilikuwa gumu. Kuchagua Kiingereza hakungefaa kwani, mbali na wasomi raia wengi hawakukijua. Hata sasa wananchi wengi bado hawajakimudu.

Serikali ilishughulikia swala hili la uteuzi. Hatimaye, Kiswahili kilitunukiwa hadhi ya kuchaguliwa. Kama lugha ya taifa, Kiswahili hutumika katika maongezi ya kawaida, mawasiliano ya kibiashara na kadhalika. Kiswahili kilichaguliwa kwa sababu kadhaa. Kwanza, baadhi ya wasomi walifikiri kwamba lugha hii ilikuwa na asili ya Kiarabu. Kwa sababu hii walifikiria kuwa Kiswahili hakikuwa lugha ya kabila lolote. Pili, wengine waliamini kwamba Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu na lugha za Kiafrika. Hivyo kingekubaliwa na makabila yote. Hata hivyo wasomi wengine walishikilia kuwa hii ilikuwa ni lugha ya Kiafrika asilia bila mchanganyiko wo wote.

Hivi leo hakuna ubishi wo wote kuhusu asili ya Kiswahili. Hii ina maana kuwa Kiswahili kimekubalika kama lugha ya kiasili Afrika Mashariki. Pia ni kitambulisho cha utaifa wa nchi kama Kenya na Tanzania. Isitoshe, Kiswahili ni lugha mojawapo ya lugha za taifa nchini Congo, Rwanda na Burundi.

41. Nini hasa kilichotatiza uchaguzi wa lugha ya taifa?
   A. Wakenya walijua lugha nyingi tofauti.
   B. Hakukuwa na lugha maalum ya kiasili ambayo ingechaguliwa.
   C. Makabila na lugha nyingi nchini Kenya.
   D. Wakenya hawakutaka kuchagua lugha ya kikoloni.

42. Kwa nini haingefaa kuchagua Kiingereza?
   A. Ilikuwa lugha ya wasomi na raia.
   B. Ilionekana lugha ngumu isiyoweza kueleweka.
   C. Si watu wengi walioweza kukiongea.
   D. Wenyeji walichukia wageni na lugha yao.

43. Kulingana na taarifa lugha ya taifa hutumika vipi nchini Kenya?
   A. Katika mawasiliano ya siasa na shughuli rasmi.
   B. Katika mawasiliano ya kawaida, biashara, siasa na dini.
   C. Katika maongezi ya kawaida na dini.
   D. Katika maongezi na mawasiliano ya serikali.

44. Kwa nini Kiswahili kilichaguliwa hatimaye kuwa lugha ya taifa?
   A. Kwa sababu uamuzi huo ulitolewa na wasomi.
   B. Kwa sababu kilifikiriwa tu kuwa ni lugha ya Kiarabu.
   C. Kwa sababu kilitumika kwingi barani Afrika.
   D. Kwa sababu kilifikiriwa kuwa si lugha ya kundi lolote.

45. Maana ya neno hatimaye ni
   A. baadaye
   B. aghalabu
   C. tena
   D. mwanzoni

46. Uliposoma habari hii ulipata jumla ya maoni mangapi juu ya asili ya Kiswahili?
   A. mawili
   B. moja
   C. matatu
   D. manne

47. Maana ya neno hadhi kama lilivyotumika katika kifungu ni
   A. heshima
   B. zawadi
   C. umaarufu
   D. ubora

48. Lugha ya taifa nchini ni muhimu kwa kuwa
   A. hutumika na watu wengi
   B. inapendwa na wananchi wote
   C. huimarisha amani na nchi jirani
   D. ni kitambulisho cha utaifa.

49. Maana ya hakuna ubishi wowote ni
   A. jambo la kujadiliana
   B. hakuna pingamizi zozote
   C. jambo lisilo wazi
   D. hakuna kufikiana tena.

50. Kiswahili ni lugha mojawapo ya lugha za taifa inamaanisha
   A. ni lugha ya kimataifa
   B. ni lugha ya kiasili
   C. kuna lugha zingine za taifa
   D. ndiyo lugha pekee ya taifa.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.*

Mwisho wa mwaka wa 1999 ulishangiliwa na kila mtu kwa uwezo wake. Jamii mbalimbali zilisherehekea kwa kuchinja mbuzi, kondoo, ng'ombe na kadhalika. Wale ambao hawakuwa na uwezo huo walichinja kuku. Mradi kila mtu alishangilia. Vigelegele, nderemo na shangwe kote! Vijana walirusha baruti angani ilhali wachezaji walicheza densi na nyimbo za kitamaduni. Wakristo nao walishangilia kwa maombi makanisani huku Waislamu wakitoa shukrani zao kwa Allah misikitini.

Katika shangwe hizi zote watu wengine walijawa na hofu nyingi moyoni. Je, tarehe moja ya karne mpya ingekuwa siku ya aina gani? Baadhi yao walidhani ingekuwa mwisho wa dunia! Wapo, bila shaka, waliokesha usiku huo ili mwisho wa dunia usiwafikie wakiwa usingizini.

Miezi kadhaa, kabla ya mwisho wa mwaka, ilitangazwa kuwa mwisho wa karne ungeleta hitilafu kwenye mitambo ya kompyuta. Pia, ilitangazwa kwamba shughuli zote zinazoendeshwa kwa utaratibu wa kompyuta zingesimama. Je, shughuli za benki? Wateja wa benki walitaharuki na wengi wakatoa pesa zao kwenye benki na kuzitafutia mahali pengine pa kuzihifadhi. Pengine baadhi yao walizika pesa zao ili kuzinusuru na wengine wakazishonea ndani ya matandiko. Lakini wasiwasi huu uliwapata tu waliokuwa na akiba kwenye benki. Wale ambao hawakuwa nazo hata habari walikuwa hawana.

Mara nyingi watu hujitia wasiwasi wa bure, wasiwasi usio na msingi. Pengine haya yote ni hali ya kibinadamu.

31. Mwisho wa mwaka wa 1999 ulishangiliwa
   A. kwa kuchinja ng'ombe, kondoo na kuku
   B. kwa kuchinja kulingana na uwezo wa mtu binafsi
   C. kwa kuchinja mbuzi na kuku
   D. kwa jamii mbalimbali kuchinja ng'ombe.

32. Kwa nini kulikuwa na vigelegele na shangwe kote?
   A. Kwa sababu ya kurusha baruti angani.
   B. Kwa sababu ya kuukaribisha mwaka mpya.
   C. Kwa sababu ya maombi makanisani na misikitini.
   D. Kwa sababu ya densi na ngoma za kiasili.

33. Ni wazo gani lililowajaza watu hofu moyoni?
   A. Kwamba mwisho wa dunia wangekuwa bado usingizini.
   B. Kwamba tarehe moja wangekuwa wakikesha usiku.
   C. Kwamba katika shangwe hizi mwisho wa dunia ungefika.
   D. Kwamba tarehe moja ingekuwa mwisho wa dunia.

34. Hitilafu kwenye mitambo ya kompyuta
   A. ingesimamisha kuendeshwa kwa utaratibu wa kompyuta
   B. ilitangazwa mwisho wa karne kwenye mitambo ya kompyuta
   C. ingesimamisha shughuli zote zinazohusika na kompyuta
   D. ilitangaza shughuli zilizoendeshwa kwa utaratibu.

35. Baadhi ya wateja wa benki
   A. walitoa pesa benki na kuzihifadhi kwingine.
   B. walitoa pesa benki na kujishonea matandiko yao.
   C. walitoa pesa na kuzihifadhi kwa wengine.
   D. walitoa pesa na haijulikani kama walizizika.

36. Walitaharuki ina maana
   A. waliingiwa na hofu
   B. walipigwa na butwaa
   C. walijawa na furaha
   D. waliingiwa na hasira.

37. Kulingana na habari hii maana ya kuzinusuru ni
   A. kuzishonea
   B. kuziokoa
   C. kuzizika
   D. kuzitoa.

38. Sentensi 'wale ambao hawakuwa nazo, hata habari walikuwa hawana' ina maana kuwa
   A. wale ambao hawakuwa na pesa benki hawakujua kungekuwa na sherehe.
   B. wale ambao hawakuwa na pesa benki hawakuwa na kompyuta.
   C. wale ambao hawakuwa na pesa benki hawakujua kuwa mitambo ya kompyuta ingekwama.
   D. wale ambao hawakuwa na pesa benki kompyuta zao hazingekwama.

39. 'Wasiwasi usio na msingi' ni
   A. wasiwasi usio na sababu
   B. wasiwasi wa mwisho wa mwaka
   C. wasiwasi wa hali ya kibinadamu
   D. wasiwasi wa akiba iliyowekwa benki.

40. Kichwa kinachofaa zaidi kwa habari hii ni
   A. vigelegele, nderemo na shangwe
   B. hitilafu ya benki na kompyuta
   C. mabadiliko ya karne mpya
   D. sherehe za mwisho wa karne.